**Learning by Ear 2009**

Media & Information

Author: Hope Azeda

Redaktion: Ludger Schadomsky

Kisuaheli Translation: Eric Ponda

**EPISODE 2**

*CHARACTERS: Wahusika*

| | |
|---|---|
| Announcer: | Male/female |
| "Young Junior" | Male, 15 years old |
| "Sister P." | Female, 16 years old |
| "Charlie" | Male, 18 years old |
| "Ezra": | Male, 22 years old. Brother to "Young Junior". |
| "Mr.T": | Male, 30, sound technician |

**INTRO:**

Karibu msikilizaji kwa makala nyingine ya mfululizo wa vipindi vyetu vya Learning By Ear "Noa Bongo jenga maisha yako" tukizungumzia sekta ya habari na Vyombo vya habari. Na kukugusia tu yaliyojiri katika kipindi kilichotangulia, Sister P, Young Junior na Charlie ni waasisi wa klabu marufu ya muziki ya *Dot.Com.Club.* Na wote wameelekeza juhudi kutimiza ndoto yao katika fani hii ya muziki. Lakini mambo hayaendi kama wanavyotarajia hasa baada ya kituo

cha redio ya taifa kukataa kucheza muziki wao.Hali hii inawalazimu wahusika kwenda mapana na marefu kutimiza ndoto hiyo. Karibu nikitumai utaufurahia mchezo huu!

EPISODE 2

SCENE 1

SFX: ***In the studio, a keyboard is playing hot R&B samples for some 15 seconds and then it suddenly stops.***

1. **Mr T:** Damn! Jamani , ni nini? Sister P,….ni nini mbaya?

2. **Sister P:** Pole Mr T, nimekosea tuanze tena. Young J, Charlie, tumakinike tafadhali.

3. **Young J:** Sio hivyo! Nani ambaye hana makini? Usimfanye Mr T afikirie ni makosa yetu.

4. **Mr T:** Young J, nilikupa ishara mara tatu uianze kuimba lakini wewe.. -

   **(sfx a hold on keyboard notes)** na unabaki kunitazama tu kama sungura muoga.. (**Losing his temper)** Sasa unataka nifanye nini?

**5. Young J:** Sawa , saaaawa Mr T,usitukasirikie!. Ni muziki wetu na pia ni pesa zetu.Hatuko hapa bure, hii studio tumelipia!**.**

6. **Mr T:** Mfanye haraka, kuna watu wengi wanaosubiri, kama mko hapa kufanya mchezo mimi sina muda huo wa kupoteza, nitamfukuza studioni.

7. **Charlie**: Punguza hasira Mr T, wacha tujipange kisha tuendelee!.

8. **Sister P:** Sawa,sawa.Tunazungumza sana….tuendele. Charlie, unataka Mr T afanye nini?

9. **Young J:** Ni huo msisimko ulionao !.

10. **Mr T:** Mmsisimko wangu una nini?

11. **Young J:** Upunguze.

12. **Sister P & Young J:** Nini?

13. **Mr T:** Sasa sawa . Kama hilo ndilo tatizo nitaupunguza.

**SFX starting the key board.**

14. **Sister:** Hapana simamisha , Mr T.

**SFX Key board stops.**

15. **Sister P:** Nadhani ni vyema tukubaliane !. Young J, ikiwa ni lazima tupunguza hisia na msisimko basi wasi wasi wangu ni kwamba muziki wetu utakosa ladha.

**16. Charlie**: Ni kweli, Sister P, tukikubaliana kufanya hivyo hatari iliyopo ni kwamba muziki wetu hautakuwa tofauti ile muziki ya zamani iliyochezwa miaka ya 70. Young J, si unaijua ule muziki tunataka?. "*Tupa tumpampa tutumpa tupa"*.

**17. Sister P:** Nilidhani Mr T. atasema tupandishe hisia kidogo!

**18. Mr T:** Ehh…mimi ndie fundi wa mitambo hapa,kwa hivyo hamna budi kufuata maagizo yangu, sawa ?

**19. Sister P:** Sawa , boss!.

| **SFX Keyboard plays hot R&B tunes** |
|---|

**20. Sister P:** *Dream on ....... yeah dream and dream on x 2*

**21. All together**: " *Dream on ....... yeah dream and dream on*

*All night ........ dream on*

*All day ............dream on*

*Yeah Yeah….you hear me?"*

| **Sfx Suddenly keyboard stops** |
|---|

**22. Charlie**: ahhh, nini Mr T? Umeme umekatika?

**23. Mr T:** Hapana … muziki huu hauleti hisia zozote.

**24. Young J:** Sasa unaona? ,nilikwambi lazima tupunguze msisimko .

**25. Mr T:** Charlie, hapana si kupunguza msisimko,…changamkeni! . Sauti zenu zinasikika zimechoka, namaanisha.........

**26. Sister P:** Sasa tufanyeje?

**27. Mr T:** Tupumzike dakika 30 hivi, tujichangamshe kidogo kisha turudi kuendelea.

**End Scene one**

***In a busy, restaurant people are heard from a distance making orders, pulling chairs back and forth and some music in the background Non-stop footsteps in and out.***

**28. Sister P:** Balaa gani hii? magazeti,picha za Baba mtakatifu, Bob Marley. Kwani hili ni kanisa, kiwanda cha uchapishaji, ukumbi wa disco au ni mkahawa? Huu ni upuzi mtupu, kwani hatuwezi kupata mahala pengine pa kula?

**29. Young J:** Ni vigumu kuapata hapa mjini . Huu ndio mkahawa pekee hapa, Sister P.

**30. Charlie:** (**sniffing**) Kunaharusu ya kuvutia.Lazima chakula hicho ni kitamu sana.

**31. Sister P:** Labda nikitamu kama harufu inavyovutia.

**SFX pulling chairs and table**

**32. Young J:** Tayari nimeanza kudondokwa na mate.Lakini tatizo ni mahali pa kuketi, tutaketi wapi?

**33. Charlie:** Pale!..,hebu twende haraka karibu na ile meza ya magazeti. Wale watu wanaondoka.

**34. Sister P:** Lakini ni viti viwili tu.

**35. Charlie**: Nitaleta kiti kingine. Wewe na Sister P munaweza kukalia viti hivi viwili.Mimi ni lazima niketi mahala ambapo naweza kuona vizuri beskeli yangu

**SFX fast moving steps on the floor, pulling chairs.**

**36. Young J:** (**Yawning)** Nimechoka na pia nasikia njaa. Haya magazeti yanauzwa?

**37. Sister P:** Bila shaka !…unaweza kuchukua moja .Ndio maana ulikuwa unatusumbua studioni?.

**38. Charlie:** (**Approaching)** *Tupa tumpampa tutumpa tupa*

**39. Young J:** Charlie, Tafadhali tupe nafasi. Tutarejelea kazi hiyo baada ya kula.

**40: Charlie**: (**Whispering)** Nilitaka kujigamba mbele ya hawa jamaa zetu.Wote waligeuka kuniangalia wakifikiri mimi ni mmoja wa wale Ma-Dot.Com,ndio nikaamua kuongeza madaha na kuimba wimbo huu wa *tupa tu*. Sasa wahudumu wako wapi?

**41: Sister P:** Huduma zao ni za pole pole. Wanafikiri tuko hapa kupigwa picha . Ahhaa,ndio huyu hapa, muite!.

**42. Charlie**: Pisssssssssss, piss pisss, njoo hapa msichana!.

**43. Sister P**: Nakerwa na jinsi wasichana hawa wanavyojizungusha licha ya huduma zao mbovu.

**44. Charlie:** He...hhee… atakusikia.

**45. Waitress:** **(Broken English with strong accent)** Semeni hapa, mumeniita? Niwasaidie vipi ndugu na dada?

**46. Young J:** Picha moja inagharimu pesa ngapi hapa kwenye mkahawa wenu?.

**47. Waitress:** **(laughs)** Hapa ni mkahawani sio studio ya kupiga picha. Samahani nadhani mumekosea!.

**48. Charlie**: (**laughs)**Hivyo ndivyo unavyofikiria? Sababu ya kusema hivyo ni kwamba tangu tumeingia hapa mumekuwa mkitutazama tu kana kwamba tumekuja kupigwa picha, sivyo?.

**49. Waitress**: Kwani hii ni mara yenu ya kwanza kuingia mkahawa huu leo?

**50. Sister P:** Eti nini?

**51. Waitress:** Nawauliza hii ni mara yenu ya kwanza kuingia mkahawa huu?

**52. Sister P**: Si hoja iwe mara ya kwanza au mia moja. Mutatuhudumkia au la?

**53. Waitress**: Tafadhali usikasirike, hapa anajihudumia yaani "***safe serice***". Kila mmoja anachukua anachotaka na mimi kazi yangu ni kuodnoa vyombo vilivyotumika, kama vile chupa vikombe,sahani na kadhalika.

**54. Young J:** Oohoo, Sister P, sasa umuombe msamaha.

**55. Sister P:** Pole na akhsante sana, tutaenda kujihudumia. Tufanyeni haraka muda unayoyoma. (***Laughing)*** Umesikia hiyo, …hapa ni "***safe service***".

**56. Charlie:** **(laughing)** Sister P, usianze kumkejeli, amejaribu angalau kuwasiliana nasi.

**SFX as they talk, a radio gets louder and Beethoven is being played on the lunch time music programme.**

**57. Sister P:** Aah, hiyo bila shaka ni redio yetu ya taifa

**58. Young J:** Bila shaka!.Ni wapi kwengine unaweza kusikia muziki huo isipokuwa tu kupitia redio ya Babu yako.Hiyo si nyengine bali redio ya taifa.

**59. Charlie**: Muuuziki wa zamaaaani kila wakati!. Unachukiza. Hii ni changamoto kwetu.Lazima tuanzishe kituo chetu cha redio naamini baada ya kufungua

stesheni yetu hakuna mtu atakayefungulia redio hiyo ya taifa punde kituo hicho cha FM Dot Com kitakapoanza kueperusha matangazo yake.

**60. Young J:** Lakini bado najiuliza ni vipindi gani tutakavyoandaa punde ndoto ya kufungua kituo cha redio FM Dot Com itatimia.

**61. Sister P:** Tayari nimeanza kupanga ratiba ya vipindi nitakavyopeperusha hewani katika kituo hicho.Kama vile kucheza muziki ya waimbaji mashuhuri barani Africa, meli ya wapendanao, na kipindi cha usiku mwema. Usinifanye nikashikwa na wazimu kwa hamu hiyo ya kuwa na kituo hicho.Kwani tayari nishaanza kufikiria miziki nitakayocheza. Aha! Pia nitataandaa kipndi cha kumi bora.

**62. Young J:** Tunaongea hapa na chakula kinaisha!. Twendeni tukachukue chakula na kisha baada ya kula nitamwambia maoani yangu kuhusu kituo hicho.

**63. Charlie:** Ni nini , Young J?

**SFX pushing chair and table as they stand up**

**End scene two.**

SCENE 3

| |
|---|
| **SFX: On the verandah, on a slightly busy street, a few vehicles people and motor cycles pass.** |

**64. Charlie:** "*Tumpa tumpampa tumpa".*

**(Sfx trying to open the door)**

Ehhe sasa mnaweza kusahau mambo kurekodi… Kumefungwa!.

**65. Sister P:** Kwanini Mr T anafaya hivi ? Ametwambia turudi baada ya muda mfupi na sasa ametoka!. Mimi nachukua watu wanaojigamba kama wababe na anjifanya kujua kila kitu kama *Nepoleon!.*

**66. Young J:** Labda pengine pia emekwenda kula. Sawa, wakati tukimsubiri Mr T,nini mawazo yenu kuhusu suala hilo?

**. Charlie**: Suala gani?

**68. Young J**: Namaanisha suala la kuanzisha Gazeti la **DRILL THE BRAINS**. Badala ya kituo cha redio tunaweza kuanzisha gazeti, sijui lakini mimi mawazo yangu yako kwa gazeti.

**69. Sister P:** *Come on*, Young J. Kwanini unataka kujiingiza katika shughuli ya uchapishaji magazeti? Hakuna jipya katika uandishi wa magazeti .Wewe

mwenyewe ulishuhudia jinsi magazeti yanavyosika vumbi pale mkahawani.Hakuna anayejali!.

**70. Charlie:** Binafsi sioni mradi huu wa uchapishaji magazeti utakuwa wa manufaa kwetu. Kanini fikra hizi zimekutawala?

**71. Young J:** Tangu uanze kuzungumzia suala kuanzisha kituo cha redio, nimekuwa nikifikiria sana,umuhimu wake, gharama na kadhalika.Mimi naona mradi wa kuanzisha gazeti ni bora kuliko redio ambayo kila mmoja amechoka nayo.

**72. Sister P:** Unamana kuwa tukianzisha gazeti tutaweza kuchapishwa kuziki wetu katika gazeti hilo badala ya kuimba?

**73. Young J:** Kimsingi, tunatafuta chombo cha gharama nafuu na kitakachowavutia vijana kama sisi. Tunahitaji kuanzisha mambo yanayoenda na wakati na kizazi cha sasa..

**74. Charlie:** Hasa..! hivyo ndivyo tutakavyo.

**75. Young J**: Kwa kutumia elimu yangu ya hesebu na masuala ya uchumi, naona kwa kuzingatia rasilimali chache tulizonazo,gazeti ni chombo cha gharama nafuu.Katika gazeti hatuhitaji kufungua ofisi au studio. Tunachohitaji ni kifaa kinachofahamika kama *flash disk*, na kwenda kwa kampuni ya

uchapishaji.Lakini redio tunahitaji studio na vifaa vingine ….!

**76. Charlie:** Pengine mawazo yako ni mazuri,lakini kwangu mimi naona ni gharama kuanzisha gazeti kuliko redio. Je umefikiria kuhusu mahala pa kuyahifadhi magazeti hayo na gharama ya kuyasambaza?

**77. Sister P:** Labda pengine uyahifadhi chini ya kitanda chako, gazeti linachangamoto nyingi. Nilazima utafute majenti wa kuyasambaza na kadhalika.Lakini redio huna shida zote hizo. Unachotoa ni hewa na itamfikia kila mmoja katika pembe zote za nchi, na ni habari za kila aina bila ya kufikiri gharama ya ugawaji.

**78. Charlie**: Na hii ndio sababu kampuni nyingi za magazeti zimefilisika.Hatutaki aibu.Mara nyingine utakuta gazeti lilichapishwa mwezi Januari na bado linauzwa mwezi Juni.

**79. Sister P:** Mbali na hayo watu ni wavivu kusoma hapa nchini.Ni wachache sana ambao wako tayari kutumia pesa zao kununua gazeti .Habu tazama kiwango cha watu wasiojua kisoma na kuandika humu nchini.Ni wangapi wanaweza kusoma na kuandika? Wasomi ni wachache lakini kwa redio hilo si tatizo.

**80. Young J**: Munaongea sana na hamujafanya mazoezi.

**81. Charlie**: Labda uwe na bahati ya kuwa na wasomi wengi kama baba mdogo!.Yeye hutaka kuonyesha watu amesoma kwa kununua gazeti kila siku lakini sababu kubwa ni kutazama picha tu huku akijifanya eti anasoma. Lakini naye siku moja alipata aibu alipokutikana akisoma gezeti chini juu.

**82. Sister P:** (**laughs)** Hapa watu wetu wanamazoea ya kutumia magazeti msalani au kufunga njugu, mihogo na kadhalika.

**83. Young J:** Sitaki hata kufikiria machungu yatakayonifika kwa kuona ukurasa wa kwanza wa gazeti langu chooni.

**84. Sister P:** Sawa, Young J, sasa bado umeshikilia msimamo wako wa kuanzisha gazeti au tuendelee na wazo la redio?

**End episode**

**OUTRO**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala haya kwa leo. Ili ujue zaidi iwapo ni mradi wa gazeti au redio uliokubaliwa, ungana nasi kwa kipindi kijacho tukizungumzia mengi kuhusu habari na vyombo vya habari. Pia iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki unaweza kutembelea mtandao wetu wa LBE wa dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.